JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI KAZIMA,

S. L. P 369,

TABORA.

26/10/2021.

SIMU: MKUU WA SHULE 0629 443 071
0788 400 218

MKUU MSAIDIZI 0766 004 042

KUMB: NA _____

MZAZI/ MLEZI/ WA _____

S. L. P _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAZIMA - TABORA KIDATO CHA KWANZA 2022.

- Ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao _____amechaguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA (BWENI) katika shule hii kwa mwaka huu wa masomo 2022. Hivyo nachukua fursa hii kukupongeza saana wewe na mwanao.
- Shule hii (Kazima Sekondari) ipo Mjini Tabora. Mita 200 Kusini Magharibi ya kituo cha Reli (Tabora Railway Station) na kilomita 1.5 Mashariki ya kituo kikuu cha Mabasi Tabora Mjini – karibu kabisa na ORION TABORA HOTEL. Hivyo unaweza kusafiri toka uliko na kufika shuleni kwa Barabara (Mabasi) ama kwa Reli (Gari Moshi la abiria)
- Anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 09/01/2022 kwa ajili ya usajili tayari kuanza masomo kwa muhula wa kwanza.
- Mara upatapo barua hii na kuisoma kwa makini, tafadhali unatakiwa kumpatia mwanao mahitaji yote stahili (yaliyoorodheshwa) ili kumwezesha afike shuleni mapema bila kupoteza muda wa masomo.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. **SARE ZA SHULE.**
   Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shule akiwa na

   - Sketi (2) mbili za rangi ya damu ya mzee zenye marinda kuzunguka sketi yote marinda ya ukubwa nchi 2, ziwe ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu.
   - Gauni ya rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya kushindia na kufanyia kazi nje iwe ndefu kukaribia fundo la mguu mshono wa solo.
   - Sweta (2) za rangi ya damu ya mzee.
   - Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi.
   - Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vya ngozi jozi mbili (2).
   - Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2)
   - Truck suit damu ya mzee.
   - Raba za michezo.
   - Shuka mbili (2) rangi ya blue bahari (light blue) pamoja na mto na foronya zake.
   - T-shirt ya rangi ya damu ya mzee haina kola
   - Tai ya rangi damu ya mzee.
   - Blanketi la kijivu kwa anayehitaji.
   - Sketi ya mchezo wa mpira wa pete rangi ya damu ya mzee inayoishia magotini, inayofungwa kwa kamba ya damu ya mzee

Mwanafunzi wa kiislamu anatakiwa kuja na

- Sketi ndefu hadi kuvuka vifundo vya miguu rangi kama zilivyo onyeshwa hapo juu, marinda makubwa mbele na nyuma na mawili kila ubavu.
- Nusu kanzu nyeupe (2) zisizo bana wala kuonyesha kwaajili ya darasani, ziwe ndefu kuvuka kiuno.
- Gauni la damu ya mzee refu kuvuka vifundo vya miguu kwa ajili ya nje ya darasa.
- Hijabu/ juba nyeupe inayovuka kiuno kwa ajili ya darasani na rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya kushindia.
- Vitu vingine ni kama vilivyoonyeshwa hapo juu.

2. **VIFAA VINGINEVYO.**
   Mwanafunzi ajapo shuleni aje na

   - Godoro moja (1) la inchi $2\frac{1}{2}$ kwa nne/ sita.
   - Sanduku la chuma la kuhifadhiwa vitu vyako.
   - Madaftari makubwa 15 kwa ajili ya masomo
   - Vitabu vya masomo yote kama kuna uwezekano.
   - Dictionary ya English – Swahili (1)
   - Ndoo ya lita 10 kwa ajili ya kufulia.
   - Sahani, bakuli, kijiko na kikombe kwaajili ya chakula
   - Pamoja na vifaa vingine vinavyomhusu mtoto wa kike.
   - Mswaki na dawa ya meno, sabuni, mafuta ya kupaka.
   - Chandarua
   - Fedha ya matumizi yake binafsi, ikiwemo ya matibabu na mengineyo.
   - Blanketi la rangi ya kijivu

NB : Kwa mwanafunzi asiyekuwa na Bima ya Afya, aje na Tsh 50,400/= kwa ajili ya BIMA YA AFYA.

3. **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.**
   Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

   (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare husika ya shule wakati wote.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za umma.
(j) Ni lugha ya kiingereza tu inayotumika uwapo shuleni.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) Kuwa na simu ya mkononi
m) Kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
n) Kutokuwepo shuleni baada ya saa kumi na mbili (12:00) jioni.

Karibu sana!



E.N MASANJA

MKUU WA SHULE



PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
TABORA MUNICIPAL COUNCIL

KAZIMA SECONDARY SCHOOL
P. O BOX 369
TABORA
_____

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

This form must be completed by a Government Medical Officer.

Student's full name _____

Present age _____

Blood Test _____

Stool Examination _____

T.B test _____

Asthma _____

Eye Disorder _____

Nose disorder _____

Ear Disorder _____

Skin Disease _____

Anaemia _____

Chest _____

Operations _____

Serious Accidents _____

Any other infections disease _____

Pregnancy _____

Additional information e.g Physical defects or impairment, chronic or family diseases etc

_____

_____

I certify that I have personally examined Mr/ miss _____ and found him/ her fit unit to purpose studies

Signature _____

Designation _____

(Official rubber stamp) _____

SHULE YA SEKONDARI KAZIMA

A. FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI _____
2. TAREHE YA KUZALIWA _____
3. MZAZI/MLEZI _____
4. UHUSIANO NA MLEZI _____
5. MAHALI ANAPOISHI MZAZI/MLEZI, MKOA _____WILAYA _____MTAA/KIJIJI_____
6. MAWASILIANO YA MZAZI/MLEZI _____
7. KABILA _____ DINI _____
8. KAZI YA MZAZI/MLEZI _____
9. WAZAZI WAKO HAI AU WAMEFARIKI (WEKA ALAMA YA ✓)
    - BABA (AMEFARIKI) ( ) BABA YUPO HAI ( )
    - MAMA (AMEFARIKI) ( ) MAMA YUPO HAI ( )
10. NDUGU WENGINE WA KARIBU NA MZAZI/ MLEZI AMBAO WANAWEZA KUTUMIKA KAMA WALEZI WA WANAFUNZI KAMA MZAZI/ MLEZI HUSIKA HAYUPO.
    (a) _____ MAHALI _____
    (b) _____ MAHALI _____
    (c) _____ MAHALI _____
    (d) _____ MAHALI _____

B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi (jina la mwanafunzi) _____ nimesoma na kuelewa sheria kanuni na taratibu za shule ya bweni, na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapo kuwa shuleni hapa kama mwanafunzi. Nitakapo kiuka kipengele chochote cha shule adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

_____ _____

Saini ya Mwanafunzi **Mkuu Wa Shule**

FOMU YA MZAZI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI MAELEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

Mimi _____ mzazi/ mlezi wa mwanafunzi _____ nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na nimekubaliana nazo kama mzazi wa wa mwanafunzi na niko tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelekezo yatakayotolewa na shule.

_____

Mzazi/ mlezi wa mwanafunzi.